# TANZANIA **MARKETS PAN**
## Masoko ya Kitanzania-PAN

Athari za vizuizi vya ushuru na visivyo vya ushuru katika kuuza mazao makuu ya chakula, kwa ustawi wa wakulima wadogo.

### Maeneo muhimu

- Kuunganisha wazalishaji na masoko, ni kitendo muhimu sana kwani kinachochea uzalishaji katika kilimo. Wakulima wasiwekewe vikwazo vya kufikisha mazao yao kwenye soko.
- Kuna makubaliano ya jumla miongoni mwa wadau, wakiwemo: wakulima, wafanyabiashara, watoa huduma, na jumuia ya wabia katika maendeleo kwamba vizuizi vya biashara ya mazao kwenye mipaka ya nchi viondolewe. Suala hili lipewe kipaumbele.
- Vizuizi vya kibiashara vimesababisha kupungua kwa asilimia hamsini mapato yao, hivyo kuwalazimisha kuhamia katika kilimo cha mazao ya biashara, mathalani alizeti.
- Kuzuia uuzaji wa mazao nje ya nchi unasababisha mfumuko wa bei, jambo ambalo linasababisha kuyumba kwa mtiririko mzima kwenye mlolongo wa thamani. Hali hii inavunja moyo wakulima na wadau wengine wenye nia ya kuwekeza katika uzalishaji, uchukuzi, na kujenga maghala ya kuhifadhia mazao.
- Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) hajawahi kufanikiwa kutekeleza jukumu lake la kudhibiti bei, wala kuwa na uwezo wa kununua chakula kinachokosa soko mahali pengine. Sababu kubwa ni urasimu uliokithiri, uwezo mdogo kifedha, kuingiliwa kisiasa, na udhaifu kiutendaji.
- Mlolongo wa thamani katika mazao makuu ya chakula huathiriwa na upotevu mkubwa wa sehemu ya mazao hayo, tangu hatua ya kuvunwa hadi kufikishwa sokoni. Upotevu huo husababishwa na magonjwa, wadudu waharibifu, uzembe wa kuyahifadhi na kuyasafirisha. Hali hii huwa mbaya zaidi Serikali inapozuia biashara ya mazao nje ya nchi.
- Sera zisizotabirika kuhusu biashara ya mazao ya nafaka nje ya nchi, huwavuruga sana wazalishaji. Hali hii licha ya kusababisha mfumuko wa bei, pia husababisha wazalishaji washindwe kuandaa mipango imara ya muda mrefu.

### *UTHIBITISHO WA MATOKEO YA MABADILIKO HASI YA SERA*

### Utangulizi

Kwa nia ya kupambana na viashirio vya uhaba wa chakula ambavyo zaidi husababishwa na hali mbaya ya hewa, Serikali imekuwa na sera ya kuzuia uuzaji wa aina kuu za vyakula nje ya nchi. Hufanya hivyo kwa kisingizio cha kuhakikisha taifa lina chakula cha kutosheleza mahitaji ya wananchi wakati wote. Aidha, Serikali inaamini kwamba vizuizi hivyo ni hatua ya kuwa na chakula kingi nchini na kuwawezesha walaji wamudu bei yake.

Uwepo wa vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya nchi na vikwazo vya kibiashara na makusudio yake, yaliibua mijadala mikubwa. Miongoni mwa masuala yaliyoibuka katika mijadala ni la kisera. Kama vizuizi hivyo vinaboresha mlolongo wa thamani ya mazao ya mahindi na mpunga, na hivyo kuongeza hamasa ya wazalishaji wa mazao haya. Mwongozo huu wa mabadiliko ya sera ni mchango kwenye mjadala huu kwa kutoa vielelezo vilivyofanyiwa utafiti ili kubaini athari zinazotokana na vizuizi vya kusafirisha mazao nje.

Mwongozo wa mabadiliko ya sera unatetea uondoaji wa vizuizi vyote katika mlolongo wa thamani ya mahindi na mpunga. Unabainisha kwamba lengo la kufikia uhakika wa chakula unaweza kufikiwa kwa kutumia njia zingine mbadala, hasa zile ambazo zinatoa motisha ya kuongeza **uzalishaji na tija**. Hata hivyo, kuwapa wakulima uhuru wa kuchagua wapi wauze mazao yao ni motisha kubwa katika uzalishaji wenye tija.

### Usuli

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, kinachangia asilimia 24.6 ya Pato la Ndani la Taifa, na asilimia 26 ya Mapato ya Fedha za

Supported by: AGRA Growing Africa's Agriculture

Kigeni. Kilimo kinatoa ajira kwa zaidi ya asilimia 75% ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi. Serikali inatambua fika umuhimu wa kilimo, ambapo katika sera zake za kitaifa na katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania (Tanzania Development Vision) ya mwaka 2025 ya Tanzania. Vilevile inatambua kwamba kilimo ndicho muhimili mkuu wa uchumi wa taifa letu, na tegemeo kuu la maisha ya asilimia kubwa ya wananchi.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza UmaskiniTanzania (MKUKUTA)[1] unabainisha wazi wazi nafasi ya kilimo katika maendeleao ya uchumi wetu. Ili kuweka mkazo kuhusu umuhimu wa kilimo, mnamo mwaka 2009 Serikali ilizindua azma ya "Kilimo Kwanza" kwa lengo la kuhamasisha wadau wote katika sekta ya kilimo, pamoja na jamii nzima ili wajumuike pamoja kukipa kilimo kipaumbele na kutambua kwamba kilimo ni suala mtambuka linapaswa kuhusisha taasisi zote katika kusukuma mbele maendeleo ya taifa kwa wakati huu, na baadae, pamoja na kupaaisha kiwango cha ustawi wa wananchi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo, na hatua zilizochukuliwa hadi sasa, mwenendo wa sekta ya kilimo nchini Tanzania unatia wasiwasi. Kwani ukuaji wake unasuasua. Katika kipindi cha miaka kati ya 2000 na 2008, kiwango cha kukua kwa sekta ya kulimo ilikuwa asilimia 4.4; kiwango hicho ni kidogo sana ukikilinganisha na lengo la MKUKUTA la asilimia 10 ifikapo mwaka 2011. Ukuaji mdogo unachangia kwa kiasi kikubwa hali ya umaskini wa wananchi, hasa wale wanaoishi vijijini. Vikwazo anuai vya kuuza mazao nje (vya ushuru na visivyo vya ushuru) vilivyobainishwa katika kiambatisho namba 1, vinadumaisha maendeleo ya masoko na kukatisha tamaa harakati za wakulima kuongeza uzalishaji.

**KIAMBATISHO 1: Aina mbalimbali za vizuizi vikuu vya kibiashara.**

- ***Vizuizi vya barabarani:*** Hivi ni vizuizi vya ukaguzi na mizani za kupima mizigo. Wafanyabiashara huchukulia vizuizi hivi kama adha kubwa ambayo husabisha ongezeko la gharama za uendeshaji kwa ucheweleshaji mkubwa wa mazao kuelekea kwenye soko.
- ***Tozo /ushuru:*** Wadau wengi wanafahamu kwamba ushuru ni chanzo cha kipato kwa Halmashauri za Wilaya kwa manufaa ya jamii. Hata hivyo, yako matatizo na malalamiko mengi ambayo budi yashughulikiwe kwenye ngazi ya taifa. Hasa tofauti ya ushuru kati ya wilaya na wilaya, pamoja na utaratibu wa kukusanya ushuru na jinsi makusanyo hayo yanavyodhibitiwa. Ukosefuwauwazikatika michakatoyoteyauchukuzi inaonekana kuwa ni tatizo. Pia, ushuru ambao huchukuliwa kama njia mbadala ya kuingiza kipato, badala ya kuwa njia mojawapo ya mapato ya Serikali, kwa mfano: ada ya kupata leseni ya biashara.
- ***Vizuizi vya kusafirisha mazao nje, na vikwazo katika vituo rasmi mipakani:*** Tanzania ina fursa tele za kufanya biashara na nchi jirani, hasa kuhusu mazao ya chakula kama mahindi, maharage na mchele. Vizuizi vya kusafirisha nje ya nchi mazao ambavyo huwekwa mara kwa mara na Serikali pindi ikihisi kuna uhaba wa mazao haya kutokana na sababu mbalimbali, kama ukame wa kipindi kirefu, hupelekea wafanyabiashara kupitapita kwa wakulima katika maeneo yenye neema na kununua mazao kwa bei chee, kupitisha mazao hayo kwenye njia zisizo rasmi, hatimaye kupandisha bei ya bidhaa hizo. Aghalabu maeneo haya yanayopakana na nchi jirani, hayajaunganishwa na masoko ya karibu nchini mwetu. Vituo vikubwa vilivyo na walaji wengi (mathalani Dar es Salaam na Arusha) viko mbali sana na sehemu za uzalishaji.



**KIAMBATISHO 2: Msimamo wa Tanzania kuhusu Umoja wa Biashara ya Kikanda:**

Mashirika ya EAC, COMESA na SADC yako katika harakati thabiti ya kuunganisha biashara ya kikanda na kurahisisha kufikisha mazao kwenye masoko. Tanzania inatakiwa kuwa na msimamo wa kuwa gwiji zaidi kuliko kulalamikia mfumo wa biashara huria mipakani ulioainishwa. Hatimaye mchakato huu utafungua fursa ya kufikia soko kubwa la kikanda kwa manufaa ya wakulima wa Kitanzania.

1 MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania). Huko Zanzibar unafahamika kwa jina la: MKUZA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar).

Tanzania ina utajiri mkubwa wa rasilimali katika sekta ya kilimo usiotumiwa, au umetumiwa kwa kiwango kidogo sana. Mbali na kumaizi nafasi ya sekta ya kilimo katika uchumi wa taifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 inatambua kuwepo kwa tija ndogo na wangu isiyotabirika, mambo yanayochangia kutetereka kwa sekta ya kilimo na ajira katika sekta hiyo. Kwa hiyo, sera zinazolenga kuongeza tija, zitakuwa na maana zaidi na athari kubwa katika kutatua changamoto halisi za sekta ya kilimo, kwa kuongeza mchango wa taifa katika biashara ya kikanda, na kuleta athari chanya katika harakati za uhakika wa chakula, kinyume na sera zilizopo zinazobana ustawi wa biashara.

Vikwazo vya kusafirisha nje ya nchi vyakula vya vikuu, hasa vinavyowekwa na watoa maamuzi serikalini, ni suala kuu lililotazamwa kwa makini katika mwongozo wa sera. Uthibitisho uliopo unabainisha kwamba makusudio haya maalum yanachukuliwa kama njia ya: 1. Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za mahindi na mpunga; 2. Kupunguza bei za ndani za mazao haya; (3) Kuongeza kwa muda kuwepo uhakika wa chakula kwa wananchi wengi. Zaidi ya haya, kuondoa udhaifu uliopo katika ufanisi kwenye kilimo, kitu ambacho ni kikwazo kwa wakulima kuongeza uzalishaji na tija.

Vilevile, vizuizi vya kusafirisha nje ya nchi mazao ni kinyume na mpango wa kiuchumi wa taifa uliobainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo hadi mwaka 2025. Kinyume hiki kinasababisha athari hasi katika ukuaji wa kilimo, na hivyo kudumaza bidii za kupunguza umaskini. Aidha, sera hizi zinarudisha nyuma kasi na mafanikio yaliyopatikana kutokana na marekebisho ya kuboresha masharti ya biashara na uwekezaji.

**Ili kufanikisha upunguzaji wa umaskini miongoni mwa wananchi waishio vijijini, sharti bidii madhubuti zichukuliwe ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao makuu ya chakula.**

## Mazingira ya Kisera na ya Kisheria

Tanzania haina waraka wowote wa kisera, wala wa kisheria, wala kikanuni wa kudhibiti biashara ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, mara nyingi Serikali husema kwamba vizuizi vyote vya kusafirisha mazao nje ya nchi si sera yake ya kibiashara. Lakini Serikali inaendelea kutumia rungu lake kudhibiti uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi kwa kigezo cha kuwepo uhaba wa chakula nchini. Mtindo wa kuweka vizuizi vya kusafirisha mazao nje unatumika kama njia ya kuhakikisha taifa lina chakula cha kutosha wakati wote. Hata hivyo kuna sera zingine zisizokuwa za kisekta au kikanuni ambazo ni nzuri sana kwa kuchochea biashara ya mazao ya kilimo, pamoja na kuhakikisha taifa lina chakula cha kutosheleza mahitaji ya Watanzania wote.

**Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kutumia busara katika kuchukuwa hatua zitakayowezesha uzalishaji na biashara ya mazao vinashabihiana kwa manufaa ya uchumi na ustawi wetu.**

## Sababu za kuzuia biashara ya mazao makuu ya chakula mipakani

Serikali mara kwa mara huweka kizuizi cha kusafirisha na kuuza chakula nje ya Tanzania,ili kuhakikisha hapatokei upungufu wa chakula nchini, hasa mahindi na mchele. Kuna nyakati ambazo Tanzania hupungukiwa chakula katika baadhi ya mikoa kwa sababu ya hali mbaya ya hewa. Hali hii ikitokea, Serikali huwajibika kuweka zuio la kuuza chakula nje ya nchi kama mkakati wa kuhakikisha taifa ni salama. Inasemekana kwamba mahindi na mchele ni mazao nyeti yenye ushawishi mkubwa wa kisiasa. Waama, mahindi inakubalika kuwa zao kuu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hata hivyo mahindi ni zao lenye kuathirika sana na maamuzi ya kisiasa, umaarufu wake unafikia mahali hata kufanya mazao mengine ya chakula ambayo pia ni muhimu, mathalani ndizi na muhogo, yasahaulike.



**Kiambatisho 3: Njia mbadala na bora kuliko vizuizi vya kuuza chakula nje**

Tarehe 30 na 31 Agosti 2012, Tanzanian Markets-PAN, iliandaa mjadala wa wadau kutoka sekta ya umma na ya binafsi kuzungumzia suala la vizuizi vya kuuza mazao makuu ya chakula nje ya nchi. Katika mazungumzo hayo washiriki waliafikiana juu ya umuhimu wa taifa kuwa na uhakika wa chakula. Kisha washiriki katika mjadala huo (wakulima, wafanyabishara, watafiti, wabia wa maendeleo, wawakilishi wa Serikali na taasisi za kiraia) wakaibua suala la kuwepo njia mbadala, hizo ni:

- Kuboresha uzalishaji na tija;
- Kufanikisha na kusaidia utoaji wa teknolojia ya kuongeza thamani mazao;
- Kuboresha miundombinu (barabara na maghala);
- Kuhamasisha wakulima kuhusu matumizi ya zana bora kwa kilimo cha kisasa;
- Kuandaa na mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya kilimo;
- Kuboresha mazingira ya kibiashara ili kushawishi uwekezaji katika sekta ya kilimo;
- Kushauri kuanzisha kilimo cha kibiashara mahali ambapo panafaa;
- Kuongeza uzalishaji wa ndani wa mazao kupitia mfumo wa ubia kati ya wadau wa sekta ya umma na binafsi;
- Kuhamasisha Masoko ya Hisa ya Mbegu;
- Kugatua Mfumo wa Akiba ya Mbegu (NFRA);
- Kuwezesha Bodi ya Mazao Mseto ya chakula;
- Kupanua tafsiri ya uhaba wa chakula ili ijumuishe aina nyingi za mazao;
- Kushadidisha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua kwa bei shindani na kudhiti mfumuko wa bei;
- Kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya wawekezaji kwenye kilimo cha mazao ya chakula.

## Utaratibu wa kuzuia biashara ya mazao makuu ya chakula mipakani

Idara ya Usalama wa Chakula, katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ndiyo yenye jukumu la kusimamia agizo la kuzuia biashara ya mazao makuu ya chakula. Kazi ya Idara hii ni kugundua viashirio vya uhaba wa muda wa chakula, ambavyo kwa kawaida dalili kuu ni mavuno hafifu kutokana na ukame au majanga mengine. Kama patatokea upungufu wa chakula, Mkurugenzi wa Usalama wa Chakula humshauri Waziri wa kilimo, Chakula na Ushirika kusudi atangaze zuio la kuuza chakula nje. Mara tangazo la kuzuia kuuza chakula nje ya nchi, viongozi wa wilaya (Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji, Afisa Biashara na Afisa Kilimo) kwa kusaidiana na Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Forodha katika vituo vya mipakani, huwajibika kutekeleza agizo hilo.

Uamuzi wa kutangaza zuio la kusafirisha mazao nje sharti ufanyike kwa makini sana baada ya kufanyika tathmini na uchambuzi wa kina wa hali halisi katika maeneo husika. Pamoja na kutoa ushauri wa nini kifanyike. Kwa bahati mbaya, mara nyingi tamko la ghafla la viongozi wakuu kisiasa, husikilizwa sana kuliko kutafakari hali halisi katika mikoa mbali mbali. Rejea makala iliyotolewa na gazeti la Mwananchi, Alhamisi, tarehe 30 Julai 2009.

**Kwa hivyo, licha ya kupitia upya sera, mikakati, maagizo, na mikataba ya kibiashara, mazungumzo ya moja kwa moja na viongozi wa Serikali yanaonyesha bayana kwamba Tanzania haina sera inayozuia uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, bali ni matangazo yanayohalalisha kuweka vizuizi.**

## Uratibu kitaifa wa utekelezaji wa kuzuia kuuza mazao ya chakula nje ya nchi

Vilevile, jambo lililo muhimu ni uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji ya vizui vya kusafirisha mazao makuu ya chakula nje. Wazo la msingi kiini cha vizuizi hivi ni kwamba wakulima huzalisha mazao ya chakula kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya familia,basi. Kwa hivyo kilimo cha kibiashara ni kwa ajili ya watu wachache sana. Dhana hii inakwenda kinyume cha azma ya Kilimo Kwanza, na Programu ya Kukuza Kilimo Kanda ya Kusini mwa Tanzania – SAGCOT. Kwa kuzingatia hatua hizi zilizochukuliwa, kilimo kinavishwa taswira ya kibiashara, hivyo kuna umuhimu wa kutilia maanani kanuni za masoko na za kibiashara. Wakulima wadogo wadogo wanatiwa moyo kuona shughuli zao zinachukua mkondo wa kibiashara na kuna hatua za makusudi za kuhamasisha kilimo chenye tija na cha kibiashara.

Kwa umaizi huu, tabia ya kutangaza vizuizi bila kutoa taarifa mapema kusudi wahanga wapate muda wa kutosha kujizatiti, budi iepukwe ili wakulima wakubwa na wadogo, pamoja na wafanyabiashara waweze kutimiza mikataba kati yao na wateja wao. Aidha, ni

muhimu kufahamu kwamba vizuizi vya kusafirisha mazao nje vina gharama yake. Gharama ambazo kwa kiasi kikubwa huwaathiri wakulima na wafanyabiashara.

## Gharama ya vizuizi vya kusafirisha mazao makuu ya chakula nje

Licha ya kuwa vizuizi vya kuuza mazao makuu ya chakula nje ya nchi huwekwa kwa ajili ya kuhakikisha taifa linabakisha chakula cha kutosheleza mahitaji ya wananchi, kuna vielelezo[2] vilivyo wazi vinavyoonyesha kwamba vizuizi kamwe havina faida inayokusudiwa. Aidha, tafiti zisizopingika zinaonyesha kwamba kuweka zuio ni zoezi lenye gharama kubwa na halisaidii lengo la muda mrefu la kuongeza uzalishaji na kupunguza umaskini kwa wananchi waishio vijijini. Athari ya kwanza kabisa ya vizuizi hivi ni punguzo la bei ya mazao ya wakulima kama inavyoainishwa katika jedwali hapa chini, takwimu hizi ni matokeo ya mazungumzo na vikundi vya wakulima, pamoja na wadau wengine. Taarifa na takwimu hizi zinatoa picha halisi ya madhara yatokanayo na vizuizi vya kuuza chakula nje ya nchi.

## Hitimisho:

Wakulima hupata kipato kidogo, pungufu hilo hufikia asilimia 300 ukilinganisha na bei ya mahindi katika soko huru nje ya nchi. Pia, wakulima hupata hasara kubwa kutokana na upotevu na uharibifu wa mazao kwa sababu kukosa hifadhi nzuri, na ucheleweshaji katika kuyasafirisha hadi sokoni.



## Mlolongo wa thamani ya nafaka: kuanzia kwa mzalishaji hadi kwa mlaji

Kuna faida ya kufahamu wadau mbalimbali katika mlolongo wa thamani ya mahindi, yaani kuelewa mtiririko mzima wa biashara yake, na nini kinafanyika. Biashara ya mahindi hufanywa na wafanyabiashara ambao hununua zao hili moja kwa moja kutoka kwa wakulima nyakati za mavuno. Utafiti uliofanyika ulibaini kwamba manunuzi mengi yanafanyikia nyumbani kwa wakulima. Katika hali hii, wafanyabiashara hununua mahindi na kuyafirisha hadi kwenye masoko ya wilayani, mikoani, au nje ya nchi. Wafanyabiashara wana chaguo tatu: i. kuuza mazao ya wakulima katika masoko makubwa ya Dar es Salaam au kwingineko penye mahitaji makubwa; ii. kumuuzia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA); iii. kuyasafirisha na kuuza nchi za jirani. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba wakulima wenyewe hawausiki katika mlolongo wa kuuza mazao yao, wala hawajui wapi yanapelekwa mara yatokapo mashambani kwao. Hali hii huwaweka katika njia panda, na ni hasara kwao. Maelezo ya jumla yaliyojitokeza wakati wa utafiti uliofanyika:

- **Soko la Kibaigwa (Kongwa, Dodoma):** Walanguzi hununua gunia moja la mahindi kwa wakusanyaji wa mahali pale pale kwa bei ya shilingi 32,000. Mengi ya mahindi hayo hupelekwa Dar es Salaam, Shinyanga na Moshi. Huko Moshi, gunia moja huuzwa kwa shilingi 95,000. Kwa sababu ya kuwepo vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya nchi kupitia mikoa ya Kilimanjaro na Mara, bei ya gunia moja la mahindi katika soko la Kibaigwa, huteremka kutoka shilingi 32,000 hadi 25,000. Wadau wanapendekeza kwamba vizuizi viondolewa ili kuongeza ushindani miongoni mwa wafanyabiashara, jambo ambalo litaongeza bei ya nafaka na kunufaisha wakulima pamoja na wafanyabiashara.

**Jedwali:** *Bei zilitolewa kwa wakulima mahali pa kuuzia, kwa gunia moja la mahindi (kilo100), kwa utaratibu ulio nje ya ule unaotumiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Utafiti huu uliofanywa kati ya mwezi Julai na Agosti 2011*

| Bei iliyotolewa kwa mkulima | Chitego | Kirando (mauzo ya nje) | Laela, Kate | Matai | Tunduma (mauzo ya nje) | Mlowo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Soko la mahali pale | 35’000/= | | 40’000/= | 40’000/= | | 35’000/= |
| Bei ya manunuzi ya NFRA | | 25’000/= | 25’000/= | 20’000/= | 20’000/= | 20’000/= |
| Soko la nje ya nchi | | 70’000/= | 70’000/= | 50’000/= | 50’000/= | 50’000/= |

2 Athari za vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya wilaya au nje ya nchi ya Tanzania”, Utafiti ulifanywa na Kilimanjaro International, Transformational Consultancy and Training,Kwa ufadhili wa Tanzania Markets-PAN, kupitia RLDC, Dodoma, 2011. “Utafiti kuhusu chaguo za sera kwa lengo la kuongeza mauzo ya mahindi na mchele nje ya Tanzania katika Kanda ya Afrika Mashariki, sambamba na kuimarisha hali ya chakula nchini Tanzania had mwaka 2025”. Iliandaliwa na Dirk Stryker, AIRD, na kufadhiliwa na USAID Feed the Future, SERA Policy Project – NAFAKA Staples Value Chain Activity, uk. 32 kiambatisho cha 7: (Historia ya vizuizi vya kusafirisha mahindi nje ya Tanzania).

- **Mkoa wa Manyara:** Kwa mujibu wa gazeti la "Arusha Times" (tarehe 23 Julai 2011) wakulima waliiomba Serikali kuuza mazao yao nje ya nchi ili waweze kupata kipato kikubwa na kuwafanya waweze kujikimu katika mahitaji yao. Ombi la wakulima lilikataliwa kutokana na tamko la kuzuia kusafirisha mazao nje ya nchi. Hata hivyo, wakulima hao walisema kwamba vizuizi havisaidii kuhakikisha kuna chakula cha kutosha nchini mwetu, wala havisababishi kupanda kwa bei ya mazao ya wakulima katika masoko ya ndani. Makamu Mwenyekiti wa MVIWATA wa Mkoa wa Manyara alisema kwamba kabla ya kuzuiwa kuuza mazao nje wakulima mkoani Manyara walikuwa wanapata angalau shilingi 45,000 kwa gunia moja la mahindi, na baada ya kuweka zuio, bei iliteremka hadi shilingi 30,000 kwa gunia moja.

## Perception of NFRA interventions in remote areas

Mapungufu ya NFRA yanayoonekana waziwazi, ni bajeti finyu inayotengwa kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima. Na hivyo kusababisha maisha ugumu wa yao. Madhara mengine ni foleni ndefu na upendeleo fulani kwa wenye nguvu kibiashara. Wakulima wadogo na wafanyabiashara wadogo hulazimika kusubiri wiki kadhaa kabla ya kulipwa mazao yao katika vituo vya ukusanyaji vya NFRA.

*"Wiki iliyopita nilileta magunia 400 ya mahindi kwa NFRA, hadi sasa sijalipwa, na sijui lini hasa nitalipwa,"alisema Bw. Felician Sikazwe, wa Kijiji cha Kaengesa,* ***Sumbawanga Vijijini****.*



Kiasi cha deni la NFRA kinachodaiwa na wakulima pamoja na wafanyabiashara, hakikuweza kufahamika mara moja kwa sababu Meneja wa Kanda wa NFRA, Bw. Mtafya, hakupatikana ili atoe maelezo. Ila ripoti ya Benki Kuu ambayo hutolewa kila mwezi kuhusu Mwelekeo wa Kiuchumi wa Tanzania, ilisema kwamba kuanzia Agosti 2011 NFRA ilishindwa kufikia lengo lake la kununua nafaka kutokana na uhaba wa fedha, licha ya kwamba Hazina ilitoa fedha. Mwaka 2011 NFRA ililipa wafanyabiashara shilingi 35,000 kwa gunia la mahindi. Hii ina maana kwamba gharama za usafirishaji, pamoja na faida ya mfanyabiashara, vilipunguzwa kwenye bei ya NFRA. Kwa hiyo, kutokana na ukweli kwamba wakulima hawana uwezo wa kujadili kuhusu bei ya mazao yao, waliambulia kati ya shilingi 20,000/= na 25,000/=. Utafiti wa suala hilo unabainisha.

- **Soko la Laela (Sumbawanga, Rukwa):** Kabla ya kuweka vizuizi, bei ya mahindi ilikuwa juu. Kwa mfano: bei ya gunia la mahindi ilikuwa kati ya shilingi 35,000 na 38,000 shambani kwa mkulima. Baada ya kuweka vizuizi bei iliteremka hadi shilingi 25,000. Serikali ilidhani kwamba kwa kuruhusu NFRA kununua mahindi kwa bei ya shilingi 35,000 kwa kila gunia, baada ya makato pato la wakulima linaongezeka. Lakini ukweli ni kwamba wakulima hugharamia mambo yafuatayo:

  i. Usafirishaji hadi kwenye kituo cha manunuzi cha NFRA (sh.1,000 kila gunia)
  ii. Ubebaji wa kupandisha na kuteremsha gunia kwenye gari (sh.1,000)
  iii. Punguzo la kilo 1.5 la vumbi (sh.500 kila gunia)
  iv. Kupeleka gunia kwenye mizani ya kupimia (sh.1,000 kila gunia). Baada ya mfanyabiashara kukokotoa gharama hizi zote, hutenga kando faida yake, kiasi kinachobakia ndicho humlipa mkulima (kwa kawaida ni shilingi 25,000 kwa gunia).

**<u>KIAMBATISHO 4: Wakulima wa Rukwa: hadithi ambazo hazijasimuliwa..</u>**

Msimu huu wa 2011 wakulima mkoani Rukwa wameathiriwa vibaya na zuio la kuuza mazao ya chakula nje badala ya kuwaleta faraja. Kijana Geoffrey Machesha, mwenye umri wa miaka 35 na mkazi wa kijiji cha Matai, Sumbawanga, ni miongoni mwa wakulima waolio athiriwa vibaya na katazo la kuvusha mahindi ng'ambo ya nchi. Kijiji hicho kiko karibu na kijiji kiitwacho Kasesha, upande wa pili nchini Zambia. Bw. Machesha ana shamba lenye ukubwa wa eka10, mwaka 2011 alistawisha mahindi katika eka 6 na kuvuna magunia 70. Mkulima huyo alinunua magunia 130 ya mahindi kutoka kwa wakulima wengine jirani zake. Hivyo alikuwa na jumla ya magunia 200 akitarajia kupata faida kubwa atakapouza zao hili nje ya mkoa.

Akiwa mwanachama wa SACCOS, mwezi Julai 2011, Bw. Machesha alichukua mkopo wa shilingi milioni moja ili kuongeza uwezo wake wa kununua mahindi mengine kutoka kwa wakulima wenzake. "Mimi na rafiki yangu tulikodi lori ili tupeleke mahindi yetu Laela kuwauzia NFRA. Tukiwa bado njiani, tuliarifiwa kwamba zoezi la kuuza mahindi NFRA limesimamishwa". Alizungumza na huzuni sana na kuonyesha sura iliyogubikwa na kukata tamaa kutokana na sera hasi zisizotabirika, kuliko kanuni za soko ambazo hutawaliwa na "uzalishaji na mahitaji".

Machesha aliyetakiwa kurudisha mkopo wake kwa Tuinuane SACCOS ndani ya miezi mitatu, alishindwa kufanya hivyo. Akaishia kutoa ahadi zisizotekelezwa kwa mtumishi wa SACCOS anayehusika na utoaji wa mikopo, Bw. Crispin Kambenga. "Afisa huyo alitusumbua sana ili tulipe deni hilo, mara nyingi tulijitahidi kumkwepa. Tulipaswa kulipa deni mwezi Septemba, tukashindwa. Tulijitahidi hapa na pale hatimaye kufanikiwa kulilipa mwezi Oktoba." Alisema Bw. Kambenga ambaye pia aliwahi kukumbana na kesi za aina hii akiwa miongoni mwa wanachama wa SACCOS wanaopindukia 600. Wengi wao wakiwa wakulima na wafanyabiashara.

Uamuzi wa Serikali wa kutangaza vizuizi vya kusafirisha mahindi kwa jirani zetu, kama: Zambia, Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemosia ya Kongo, uliwaacha maelfu ya wakulima wa mahindi mkoani Rukwa kubaki na mahindi majumbani mwao kwa miezi mingi sana. (Rukwa ni miongoni mwa mikoa mitano inayozalisha mahindi kwa wingi sana). Katibu Tawala wa Wilaya, Sumbawanga Vijijini, Salum Shilingi, alisema kwamba wilaya hiyo ina masoko mawili tu ya kuuza mahindi: NFRA na nchi zilizo jirani nasi.

## NFRA: mtazamo tofauti

Ijapokuwa NFRA ina nafasi yake katika mkakati mzima wa biashara ya mazao mahimu ya nafaka nchini Tanzania, tunapendekeza utendaji kazi wake uboreshwe kwa lengo la kuleta ufanisi bila kuathiri maslahi ya wakulima.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti uliofanyika:
*NFRA inaathiriwa vibaya na mambo mengi: Urasimu uliokithiri, kuingiliwa kisiasa, uwezo mdogo,na ufanisi hafifu kiutendaji. Timu ya wataalamu welekezi ilipigwa butwaa kushuhudia mashehena ya mahindi yakisubiri kupimwa uzito kutokana na uhaba wa wafanyakazi, uchache wa vifaa vya kupimia, na taratibu goigoi za kupokea mazao. Tatizo la shehena ya mahindi yaliyokuwa kwenye kituo hicho, ukiuunganisha na utendaji hafifu wa wafanyakazi wa kupokea na kupima mazao, inawezekana zoezi hili likachukuwa hata miezi minne kabla halijamalizika, na wakulima kulipwa haki yao. Hali hii inaweka wakulima katika hali ngumu sana kwa sababu wanahitaji fedha haraka ili kutimiza mahitaji yao, pamoja na kununua pembejeo kwa ajili ya msimu wa kilimo unaofuatia.*

Kasoro kemkemu zinazojitokeza katika utendaji wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, zinahalalisha mabadiliko chanya. Kuna haja ya Serikali kufungua zaidi milango katika ununuzi wa mazao ya chakula. Hatua hii itaondoa gharama ambazo Serikali hutumia kusimamia taratibu za soko, na kutoa ruzuku kwa ajili ya shughuli za NFRA. Faida ya sera hii ni kwamba itatoa motisha kwa wakulima kuzalisha zaidi, na kupanua jukwaa la soko la mazao ili wakulima wanufaike kiuchumi.

Hoja zilizotolewa zinaonyesha bayana kwamba kuna haja ya kuweka sawa mwenendo mzima wa NRFA ili kuleta ufanisi unaotakiwa. Tunakiri kwamba jukumu la NFRA ni la muhimu sana, kwa hiyo ni vema chombo kiendelee kuwepo. Hata hivyo, NFRA budi ijizatiti kuondoa udhaifu wake katika utendaji wa kazi, mathalani: kuchelewesha mchakato wa kupokea na kupima mazao, na kulipa wahusika. Chombo hiki lazima kijitegemee, hakipaswi kuishi kwa kutegemea Hazina ya Taifa, pia ni muhimu kishindane na washindani wake katika mlolongo wa thamani bila upendeleo wowote kutoka Serikalini. Uamuzi wa kuuza mazao kupitia NRFA budi uongozwe na nguvu za soko, kwa mfano bei inayotolewa, na ufanisi katika kutoa huduma. Wazalishaji wasilazimishwe kuuza mazo yao NFRA eti kwa sababu chombo hiki kimehodhi soko.



## Mapendekezo kuhusu nini kifanyike

Kutokana ushahidi kuhusu hali halisi iliyobainishwa katika mwongozo huu, pamoja na uthibitisho wa hali hii uliotolewa na tafiti zingine nchini mwetu, tunapendekeza yafuatayo:

- Kwanza, Serikali iongoze mchakato wa kuweka na kuhamasisha milolongo ya thamani kwa mazao–teule ya chakula na biashara, kama ilivyobainishwa (pamoja na mambo mengine) katika kipengele 2.3 cha Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo Tanzania (ASDP), kinachoweka mkazo kuhusu kuwaunganisha wakulima na masoko kwa kupitia milolongo ya thamani, kama inavyotekelezwa na mashirika na asasi za kiraia nyingi sehemu mbalimbali vijijini.

- Pili, kuhamasisha mitazamo inayoheshimu “kanuni”, pamoja na michakato ya mauzo na sera za kibiashara ili kupunguza hali ya kutokuwepo uyakini wa bei, na mfumuko unaoambatana na hali hiyo. Hii italeta ufanisi wa utendaji, kuliko kukazania mazao-teule tu. Mitazamo hii ijumlishe:

  - vigezo dhahiri vya viwango vya ushuru;
  - vigezo bayana vya kuanzisha vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya nchi;
  - kupunguza vizuizi vya kibiashara na vikwazo vya kusafirisha mazao nje ya nchi.[3]

- Kutengemeza bei ya vyakula kwa kudhibiti uzalishaji husababisha malalamiko mengi ya wakulima, pia siyo jawabu ya kuwepo uhakika wa chakula wa muda mrefu. Mkakati huu budi utathminiwe upya kwa lengo la kuufuta kabisa. Kwani unazuia ubunifu wa wakulima na kupunguza kipato chao. Vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya nchi havitakiwi kabisa, kama ilivyoainishwa katika Sera ya Kitaifa ya Biashara (NTP) - 2003.

- Kuwezesha NFRA kununua mazao kwa bei za soko kutawapa motisha wakulima kuuza mazao yao kwa kupitia chombo hiki, kuliko kutafuta masoko mbadala nje ya nchi. Ila ili chombo hiki kifanye kazi yake kwa ufanisi, kinahitaji nyenzo za kifedha za kutosha, pamoja na msaada wa kilojistiki. Ni muhimu kuwezesha NFRA kuwa mshiriki katika shughuli za biashara ya nje kwa manufaa ya wakulima. Hii ina maana kwamba NFRA atakuwa wakala wa mauzo ya nje kwa niaba ya wakulima, badala ya kuwaachia wafanyabiashara wafanye kazi hii peke yao.

- Badala ya Serikali kukazania vizuizi vya kusafirisha mazao nje ya nchi, inatakiwa kuelekeza nguvu zake katika uboreshaji wa sera za uzalishaji na teknolojia kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula, hivyo kuhakikisha taifa lina chakula cha kutosha nchi nzima.



**Supported by:**

3 Nukuu: “Articulating and mainstreaming agricultural trade policy and support”, Ramesh Sharma & Jamie Morrison, FAO – Idara ya Biashara na Masoko, Roma 2011, Uk.302